



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BENKI KUU YA TANZANIA



2 Oktoba 2025

Taarifa ya Kamati ya Sera ya Fedha

1. Riba ya Benki Kuu (CBR)

Kamati ya Sera ya Fedha (MPC) ilikutana Jumatano ya tarehe 1 Oktoba 2025, na kuamua Riba ya Benki Kuu (CBR) kuendelea kuwa asilimia 5.75. Uamuzi huu umetokana na tathmini iliyofanyika kuhusu mwelekeo wa mfumuko wa bei ambao unatarajiwa kubakia ndani ya lengo la asilimia 3 hadi 5. Vilevile, uchumi unatarajiwa kuendelea kuwa thabiti. Tathmini iliyofanywa na mashirika ya kimataifa ya Moody's na Fitch Ratings hivi karibuni, pia ilithibitisha kuwa uchumi unatarajiwa kuendelea kuwa thabiti, kwa kuipa Tanzania daraja B1 na B+, mtawalia. Kwa muktadha huu, Benki Kuu ya Tanzania itatekeleza sera ya fedha kwa lengo la kuhakikisha kuwa riba ya mikopo ya siku 7 baina ya mabenki (7-day *interbank rate*) inabaki ndani ya wigo wa asilimia ± 2 ya CBR. Wakati huohuo, makadirio ya Benki Kuu ya Tanzania yanaonesha kuwa uchumi utaendelea kukua kwa kasi ya kuridhisha.

2. Utekelezaji wa Sera ya Fedha kwa Robo mwaka iliyoishia Septemba 2025

Utekelezaji wa sera ya fedha katika robo mwaka iliyoishia Septemba 2025 ulifanikiwa kuhakikisha uwepo wa ukwasi wa kutosha kwenye uchumi. Utekelezaji huo ulisababisha hali ya ukwasi kuimarika na kupelekea kupungua kwa riba ya mikopo ya siku 7 baina ya mabenki, na kukaribia CBR kwa muda mwingi wa robo hiyo ya mwaka.

3. Mwenendo na Matarajio ya Uchumi wa Dunia

Ukuaji wa uchumi katika nchi zilizoendelea na zile zinazoibukia umepungua kidogo katika robo ya tatu ya mwaka 2025, ingawa umeendelea kuwa imara licha ya migogoro ya kisiasa na mivutano kuhusu ushuru wa forodha. Hata hivyo, kuelekea robo ya nne, uchumi wa dunia unatarajiwa kuimarika. Mfumuko wa bei umeendelea kupungua na kufikia malengo ya benki kuu katika nchi nyingi. Kufuatia mwenendo huu, Benki kuu nyingi duniani ziliamua kutokubadili au kupunguza riba zao za sera ya fedha ili kuchochea ukuaji

wa uchumi. Mwenendo huu unatarajiwa kuendelea katika robo ya nne ya mwaka 2025. Bei za bidhaa katika soko la dunia, hususan mafuta ghafi zilipungua hadi wastani wa dola za Marekani 68 kwa pipa ikilinganishwa na robo mwaka iliyotangulia.. Bei ya dhahabu iliendelea kuwa juu, kufikia wastani wa dola za Marekani 3,354.1 kwa wakia, na zinatarajiwa kuendelea kuwa katika viwango hivyo au kuongezeka kidogo.

4. Mwenendo na Matarajio ya Uchumi wa Ndani

4.1 Mfumuko wa bei kwa Tanzania Bara ulikuwa asilimia 3.4 mwezi Agosti 2025, ndani ya lengo la nchi la asilimia 3 hadi 5 na vigezo vya mtangamano wa kiuchumi kwa EAC na SADC. Makadirio ya Benki Kuu yanaonesha kuwa mfumuko wa bei utaendelea kubaki ndani ya lengo, kutokana na utekelezaji madhubuti wa sera za fedha na kibajeti, uwepo wa chakula cha kutosha, na utulivu wa thamani ya Shilingi. Mwenendo huu utachagizwa pia na uwepo wa umeme wa uhakika, na kupungua kwa bei ya mafuta ghafi. Kwa upande wa Zanzibar, mfumuko wa bei ulipungua kutoka asilimia 4.2 hadi asilimia 4, na kubakia ndani ya lengo, kutokana na kupungua kwa bei za vyakula. Mfumuko wa bei unatarajiwa kuendelea kubaki chini ya lengo la asilimia 5.

4.2 Shughuli za kiuchumi hapa nchini ziliendelea kuimarika. Kwa upande wa Tanzania Bara, uchumi ulikua kwa asilimia 5.4 katika robo ya kwanza ya mwaka 2025, ikilinganishwa na asilimia 5.2 katika kipindi kama hicho mwaka 2024. Mwenendo huu ulichangiwa zaidi na shughuli za uchimbaji madini, kilimo, huduma za fedha na bima, ujenzi, na shughuli za uzalishaji viwandani. Benki Kuu ya Tanzania inakadiria uchumi kuendelea kuimarika, ukikua kwa zaidi ya asilimia 6 katika robo ya pili na ya tatu ya mwaka 2025. Ukuaji katika robo ya nne ya mwaka 2025 unatarajiwa pia kuwa na mwenendo wa kuridhisha. Matarajio haya yanachagizwa na uwekezaji unaofanywa na Serikali pamoja na sekta binafsi, na ongezeko la mauzo ya bidhaa na huduma nje ya nchi. Uchumi wa Zanzibar ulikua kwa asilimia 6.4 katika robo ya kwanza ya mwaka 2025, sawa na ukuaji uliorekodiwa katika kipindi kama hicho mwaka 2024. Ukuaji huu ulichangiwa zaidi na shughuli za utalii, ujenzi na kilimo. Uchumi wa Zanzibar unatarajiwa kukua kwa asilimia 7.3 kwa mwaka 2025.

4.3 Ujazi wa fedha uliendelea kuongezeka kwa kasi kama ilivyokuwa katika vipindi vilivyopita, ukichagizwa na ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi. Katika robo mwaka

iliyoishia Septemba 2025, ujazi wa fedha ulikua kwa wastani wa asilimia 20.4, ikilinganishwa na asilimia 19.1 katika robo iliyotangulia. Mikopo kwa sekta binafsi, iliendelea kuongezeka kwa kasi ya takriban asilimia 16, ikichangiwa na uwepo wa ukwasi wa kutosha kwenye uchumi pamoja na ongezeko la uwekezaji katika sekta hiyo.

4.4 Sekta ya kibenki iliendelea kuwa thabiti ikiwa na ukwasi, mtaji wa kutosha na yenye kutengeneza faida. Aidha, vihatarishi katika utoaji wa mikopo viliendelea kupungua ambapo mikopo chechefe iliendelea kupungua hadi asilimia 3.3 mwezi Agosti 2025, ndani ya kiwango kinachohimilika cha asilimia 5.

4.5 Sekta ya nje imeendelea kuimarika ikichangiwa na ongezeko la mauzo ya mazao ya biashara nje ya nchi, utalii na dhahabu, pamoja na kupungua bei za mafuta ghafi katika soko la dunia. Nakisi ya urari wa malipo ya kawaida ilipungua hadi asilimia 2.4 ya Pato la Taifa kwa mwaka unaoishia mwezi Septemba 2025, kutoka asilimia 3.8 ya pato la Taifa kwa mwaka uliotangulia. Kwa upande wa Zanzibar, ziada ya urari wa malipo ya kawaida iliongezeka hadi Dola za Marekani milioni 685.6 kwa mwaka ulioishia Septemba 2025, kutoka Dola milioni 499.0 mwaka uliotangulia, kutokana na ongezeko la mapato ya huduma, hususan shughuli za utalii.

4.6 Kuimarika huku kwa sekta ya nje kulichangia ongezeko la ukwasi wa fedha za kigeni katika uchumi na kuimarika kwa thamani ya shilingi. Shilingi ya Tanzania iliendelea kuwa imara, huku thamani yake ikiongezeka kwa asilimia 8.4 katika robo ya tatu ya mwaka 2025, ikilinganishwa na asilimia 0.7 katika robo mwaka iliyotangulia. Akiba ya fedha za kigeni iliendelea kuwa ya kutosha, ambapo mwishoni mwa Septemba 2025 ilifikia Dola za Marekani bilioni 6.7, kiwango kinachotosheleza uagizaji wa bidhaa na huduma kwa zaidi ya miezi 5, sanjari na lengo la nchi na vigezo vya kikanda kwa EAC vya miezi 4.0 na 4.5, mtawalia. Ukwasi wa fedha za kigeni unatarajiwa kuendelea kuongezeka kutokana na mauzo ya korosho na dhahabu, pamoja na shughuli za utalii.

4.7 Utekelezaji wa bajeti za Serikali katika robo ya kwanza ya mwaka 2025/26 ulikuwa wa kuridhisha kwa Tanzania Bara na Zanzibar. Mapato ya ndani yalivuka lengo kutokana na mwenendo mzuri wa makusanyo ya kodi kufuatia kuongezeka kwa utayari katika ulipaji wa kodi kwa hiyari, sambamba na usimamizi thabiti. Matumizi ya Serikali

yaliendelea kuoanishwa na rasilimali zilizopo, hali inayoakisi usimamizi madhubuti wa fedha za umma. Deni la taifa halikuwa na mabadiliko makubwa kutoka robo mwaka iliyotangulia, ambapo sehemu kubwa ya fedha zilizokopwa zilielekezwa kwenye miradi ya kimkakati ya ujenzi wa miundombinu.

5. Tarehe ya kutangaza Riba ya Benki Kuu (CBR) kwa robo mwaka inayofuata Kamati ya Sera ya Fedha inatarajia kukutana tena tarehe 7 Januari 2026, na hivyo siku ya kutangaza CBR itakuwa tarehe 8 Januari 2026.



Emmanuel M. Tutuba

GAVANA